

MKATABA WA KUPANGISHA OFISI YA BIASIARA.

MKATABA huu umefanyika leo tarahе 01 Mwezi wa NOVEMBER mwaka 2021 KATI YA BIBI SOVAI JOHN NEWA wa DAR ES SALAAM , (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGISHAJI") NA KAPARI LIMITED ya DAR ES SALAAM (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGAJI").

KWA KUWA MPANGISHAJI amekubali kumpangisha mpangaji katika NYUMBA anayoimiliki kihalali.


HIVYO BASI MKATABA huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:

1. KWAMBA MPANGISHAJI amempangisha mpangaji ofisi hiyo iliyopo Mwezi – Dar es Salaam kwa kiasi cha kodi ya Tshs. 500,000 / = kwa mwezi na kwamba fedha hizo iitalipwa kwa mkupuo kwa kipindi cha kila mwaka mmoja ambayo ni jumla ya Tsh. 6,000,000/=
2. KWAMBA mkataba huu utanza tarehe 01/11/2021 hadi tarehe 31/01/2026.
3. KWAMBA Mpangaji anatakiwa azingatie usafi wa ofisi pamoja na mazingira yake na anatakiwa aturnie nyumba hiyo kwa biashara halali .
4. KWAMBA Mpangaji anatakiwa azingatie kulipa kodi kama inavyotakiwa na kuilipa kwa wakati kama ilivyokubali wa katika mkataba huu.
5. KWAMBA Mpangaji haruhusiwi kukodisha nyumba hiyo aliyopanga kwa mtu mwingine yoyote bila hidhini ya maandisgi kutoka kwa MPANGISHAJI, na ikiwa Mpangaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi Mpangaji atamrudishi ofisi kwa MPANGISHAJI.
6. KWAMBA Mpangaji na Mpangishaji wanaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa kwa maandishi mwezi mmoja kabla.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa sahihi na MPANGISHAJI na Mpangaji mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA na SOVAYA JOHN NEWA

leo hii Tarehe 01 Mwezi NOVEMBER Mwaka 2021.

SAINI:.....

MPANGISHAJI

IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA na JACKLINE SHIRIMA

(KWA NIABA YA KAPARI LIMITED)

leo hii Tarehe 01 Mwezi NOVEMBER Mwaka 2021.

SAINI:.....

MPANGAJI

